

Dhana ya Zubu katika Nyimbo za Harusi za Waswahili: Uchambuzi wa Kisaikolojia Changanuzi

Issa Mwamzandi

Ikisiri

Zubu (au dhakari, uume) kama sehemu ya mwili wa mwanamume hufahamika kama kiungo cha kuendeleza uzazi. Pamoja na fasili hiyo, makala haya yanachukua mtazamo wa kisaikolojia changanuzi unaotazama zubu sio tu kama kiungo cha kibiolojia bali kinachoweza kuwa na viashiria mbalimbali na vyenye athari tofautitofauti. Kupitia nyimbo za harusi za Waswahili, neno zubu linabainika kama mdokezo wa maisha ya ndoa na mahusiano yanayotarajiwa na wanajamii baina ya jinsi ya kike na ya kiume. Makala yanabainisha kwamba kuwa na zubu (na vilevile kutokuwa nalo) ni njia ya kufafanua mahusiano ya yule mwenye mamlaka na, vilevile, asiyekuwa nayo katika jamii ya Waswahili. Kwa utaratibu huo, zubu limebeba viashiria muhimu vya kuwafunza maarusi namna wanavyopaswa kuishi, wao wenyewe kwanza, na kisha namna wanavyostahili kutangamana na wanajamii wengine. Mbali na kuzungumzia mahusiano ya kijinsi, viashiria vinginevyo vya saikolojia changanuzi vya woga, na ambavyo vinaendelezwa na dhana ya zubu, pia vimefafanuliwa na makala.

1.0. Utangulizi

Makala yanahusu fikra za saikolojia changanuzi iliyoendelezwa na Jacques Lacan na ambayo ina misingi yake katika saikolojia changanuzi ya Sigmund Freud na mwanafunzi wake Carl Gustav Jung. Mawazo ya Lacan yamekuwa msingi wa uchanganuzi wa ufeministi na hasa ufeministi wa Kifaransa. Kwa muhtasari, Lacan anadai kwamba baina ya mwanamume na mwanamke kuna kitu kimoja tu ambacho kinabeba na kujenga ruwaza nzima ya mahusiano yao. Kitu hicho ni “zubu” ambalo linafanua suala zima la mamlaka na uwezo. Mwanamume huzaliwa akiwa na “zubu” na hilo humfanya awe na hadhi. Mtoto wa kike kwa upande wake hujikuta na dosari kwa kulikosa “zubu” na hilo humfanya alie ngoa na kutamani kuwa nalo. Baadhi ya wafeministi wa Kifaransa wamefasiri mawazo haya na kuonyesha kuwa ngoa anayoililia mtoto huyu wa kike ya kuwa na zubu ni ya kiishara tu ya kutaka kuwa na hadhi sawa na mwanamume katika jamii. Makala inashikilia kwamba zubu linalozungumziwa ndani ya nyimbo ni kiungo halisi na kimetumika kama njia

ya kuwatia woga bwana na bibi harusi. Nyimbo hizi zimewasilishwa kwa kufahamu fika kuwa Waswahili, kama walivyo wanajamii wote duniani, wana chembechembe za woga ndani ya ng'amuzibwete zao. Pamoja na hayo, viashiria vya zubu vilivyotumiwa ili kujenga woga vina azma ya kuwashajiisha maharusi kuwa na ujasiri katika maisha yao ya ndoa. Hatimaye makala yanajaribu kubainisha kuwa binadamu wana umoja wa akili na fikra sawa popote walipo hapa duniani.

1.1 Lacan na Uguzi wa Zubu kama Msingi wa Mahusiano ya Kijinsi

Msingi wa mawazo ya Jacques Lacan (1901-1981) umeathiriwa sana na Ferdinand de Saussure aliyedai kwamba tunachokipata ndani ya lugha ni tofauti za maneno. Maneno ndani ya lugha huwa daima yanakinzana, na hilo ndilo linaloyapa maneno maana zake halisi. Kwa sababu hiyo, tunafikia maana za maneno yaliyomo ndani ya sentensi kwa kutafakari uhusiano wa maneno hayo na wala si kwa kuyatafakari yakiwa pweke. Lacan anayapanua mawazo haya na kudai kwamba kitu cha pekee kinachozitofautisha jinsi hizi mbili, pale tunapozifikiria kwa pamoja, ni "uume" au "zubu." Lacan anasema kwamba zubu ni kiashiria kinachozitofautisha jinsi na husimamia tofauti za kiishara kati ya wanaume na wanawake. Chambilecho Lacan, "Unapoliondoa zubu, basi tofauti na mahusiano yao ya kiishara huporomoka pasibakie kitu."

Dhana hii ya wanasaikolojia kulifanya zubu kuwa kiungo cha kimsingi kinachofafanua mahusiano kati ya jinsi hizi mbili ndiyo iliyowafanya wadai kwamba mtoto wa kike huwaza na kutamani kuwa na zubu kama alivyo mwanamume (Selden na wenzake, 2005). Simone de Beauvoir katika kitabu chake *The Second Sex* (1949) anadai kwamba msichana hilitamani zubu kama ishara ya kutaka maisha na hali nzuri ya maisha anayoipata mtoto wa kiume na wala si kulitamani zubu lenyewe kama kiungo cha kimwili. Huu ndio msimamo unaochukuliwa na Lacan pale anaposhadidia kwamba dhana ya "zubu" haistahili kutazamwa kisisi kama tupu halisi ya mwanamume inayoendeleza uzazi. Asemavyo Grosz (1990), fikra ya zubu ya Lacan inaazimia "kuvuta nadhari zetu kwenye natija wanazopata wanaume katika jamii ya kibabedume ambapo kuthaminiwa kwake na kuhasiwa kwa uchi wa mwanamke ni njia ya kuendeleza mahusiano ya kijamii kama inavyotarajiwa katika tamaduni zetu" (1990: 50-51).

1.2 Nyimbo/Fasihi kama Msingi wa Saikolojia Changanuzi

Makala yanatambua kuwa tangu zama za mwasisi Sigmund Freud (1856-1939), saikolojia changanuzi ni eneo linalogombaniwa hasa kutokana na njia zake za kuyazungumzia mambo batini. Uchanganuzi wa ndoto ndiyo njia kuu aliyoiipendekeza Freud ya kung'amua yale yaliyofichika kwenye

ung'amuzibwete wa mtu. Asemavyo Freud, ung'amuzibwete wa mtu huficha matamano ambayo hayawezi kubainishwa wazi, au la yafyatwe humo. Vinginevyo mawazo hayo ya batini huenda yakazua aibu na fedheha kwa yule atayeyabainisha waziwazi kwa watu.

Freud aliziona kazi za fasihi zikichukuana sana na ndoto kwani uchanganuzi wake huwa hautegemei kisemwacho kijuujuu bali hutegemea maana zilizofichika. Hali hii ni sawa na kile wanasaikolojia changanuzi wanachokifanya kwani hujaribu kusarifu yaliyofichika ndani ya ung'amuzibwete wa mtu ili kutoa tiba kwa ndwele za kisaikolojia (Schmitz, 2007).

Hivyo basi, binadamu hafahamiki kwa umbo la nje tu bali utu wake usiodhihirika na uliomo ndani ya ung'amuzibwete wake ndio unaoshughulikiwa na wanasaikolojia ili ukamilifu wa matamano yake yaliyofichika uweze kufahamika. Wasomaji na wasikilizaji nao huliwazika pindi wanaposoma au kuzisikia kazi za fasihi bila kudadisi vyanzo vya burudani inayotokana na kazi hizo. Nyimbo za harusi nazo hutoa fursa hii ya kindoto ya kuweka bayana mambo ya ndani ambayo vinginevyo ingekuwa vigumu kuyazungumzia. Hadhira nayo hufurahia mambo haya ya ugoni ambayo licha ya kufutika matusi ndani yake huwa mithili ya tiba kwa akili zilizokosa namna ya kusema yasiyosemeka hadharani.

1.3 Data na Umbo la Makala

Nyimbo zilizomo ndani ya makala zimenakiliwa kutokana na tasnifu za awali kuhusu mila na desturi za Waswahili. "Kimasomaso," kwa mfano, umetokana na tasnifu ya Mwamzandi (2002) huku nyimbo nyinginezo zikinakiliwa kutoka tasnifu mbalimbali zikiwamo ile ya Ali (2014). Hizi ni nyimbo ambazo zinajenga fasihi simulizi ya Waswahili na huimbwa kwenye hafla za harusi. Nyimbo hizi ziliteuliwa kwa makusudi na kuchanganuliwa kwa kuzingatia urejelewaji wa dhana ya zubyu ndani yake. Baadaye, nyimbo husika zilichanganuliwa huku kigezo muhimu kikiwa ni kuwapo kwa ruwaza za mada mbalimbali zilizozungumziwa na ambazo zimezingatiwa katika makala.

Katika hatua ya kwanza, makala yanaangazia fasiri ya zubyu kama inavyoendelezwa na mwanasaikolojia Jacques Lacan. Katika ufafanuzi huo, tutaangalia jinsi zubyu linavyokuwa kiashiria cha kuelewa mahusiano ya kijinsi kama inavyobainika katika wimbo wa "Kimasomaso." Hatua ya pili ya makala imefuata mawazo ya mwanasaikolojia Carl Gustav Jung na dhana yake ya ung'amuzi jumuishi wa binadamu na namna unavyohodhi sifa za woga. Kupitia nyimbo nyingine za Waswahili, makala yanafafanua jinsi viashiria mbalimbali vya zubyu vinavyoweza kuendeleza tasnifu kuu ya dhana ya woga. Pamoja na

hivyo, msingi wa woga uliomo ndani ya nyimbo hizi unalenga kuwashajiisha bwana na bibi harusi.

2.0 “Kimasomaso” kama Somo Maalumu la Saikolojia Changanuzi

Kimasomaso ni wimbo ulioimbwa na Issa Matona pamoja na kikundi cha Jeshi la Kujenga Taifa (J.K.T.). Ni wimbo unaofafanua utamaduni wa Waswahili na umesheheni mawaidha yanayogusia mahusiano ya mwanamke na mwanamume, hasa katika maisha yao mapya ya ndoa wanayotarajia kuyaanzisha kama mke na mume nyumbani. Katika sehemu hii, basi, ninadhamiria kuchanganua jinsi dhana hii ya zubu inavyokuwa msingi wa mahusiano kati ya jinsi hizi mbili hasa kwa namna woga unavyojengwa. Nimechagua beti mbili tu za wimbo mzima ambazo, kwa muhtasari, zinatolewa kama ushauri kwa bibi harusi na jinsi atakavyowakaribisha wageni wa aina na aila mbalimbali, akiwamo mumewe. Katika ubeti mmojawapo, tunaelezwa yafuatayo:

*Somo yake bi arusi hebu nitafutieni
Na kungwi lake arusi waje hapa uwanjani
Tuje tumfunze mwari malezi ya kizamani
Unapopelekwa kwako mama unapofika nyumbani
Ukacheke na mumeo mama umpumbaze chumbani
Wakaja na ndugu zako uwakaribishe nyumbani
Wakaja mawifi zako mama uinuke kitandani
Wanapokuja wakwezo uwaweke ukumbini
Wakaja shemeji zako uwaweke barazani
Wakaja mashoga zako sema nao dirishani*

Chanzo: Mwamzandi (2002)

Ubeti huu unaanza na wito wa mwimbaji kutaka atafutiwe “Somo” na “Kungwi” wake bi arusi ili waje uwanjani kwa azma ya kumfunda mwari maisha ya ndoa. Umuhimu wa “Somo” na “Kungwi” katika kumpa bi harusi mafunzo ya unyumba umezingatiwa kwa mapana katika tafiti mbalimbali (taz. Mwamzandi, 2002; Ntarangwi, 1998). Katika maisha ya msichana Mswahili, somo huwa mhusika muhimu sana wa kuhifadhi siri na mambo ya ndani ya msichana huyo. Wakati mwingine, somo humfunza msichana huyo upishi, kujisitiri wakati wa hedhi, ususi na kazi nyingine za nyumbani. Wakati mwingine hutokea kuwa somo yake harusi anafahamu siri nyingi kuliko hata mama mzazi wa msichana huyo. Kungwi naye ni mwalimu wa mila na utamaduni wa Waswahili ambaye jukumu lake kubwa ni kumkomaza mwari. Huyu humfunza bibi harusi namna ya kuishi na mume katika kipindi cha tangu kuletwa kwa posa hadi siku chache baada ya mwari kuolewa. Ni katika

muktadha huu ambapo mwimbaji wa “Kimasomaso” anawaita walimu hawa wa kitamaduni ili wazidi kumpa mawaidha bibi harusi ya namna ya kuwakaribisha wageni wake. Makaribisho haya, hata hivyo, yanaathiriwa sana na kile ambacho nimekirejelea hapa kama “siasa za zubu.” Ninachomaanisha ni kuwa makaribisho yanayohimizwa yanahusu na kuathiriwa moja kwa moja na tupu halisi aliyonayo mtu. Unapouchanganua ubeti huu kwa makini, ni dhahiri kuwa kiungo hiki kimetiliwa manani sana katika makaribisho yaliyopo. Ni kana kwamba mwimbaji anafahamu fika namna zubu linavyoweza kuwa chanzo cha ama kudumisha au kuiharibu ndoa ya bibi harusi. Mafunzo haya hayabainishi hilo waziwazi ila bibi harusi anatarajiwa awe na umaizi wa semantiki iliyofichika humo. Hebu tuone katika baadhi ya mishororo maalumu, siri na hekima anazopewa bibi harusi kuhusu wamiliki mazubu, yaani wanaume na namna anavyostahili kutangamana nao.

2.1 Wanaume wenye Mazubu yenye Hatari

Kwako mama unapofika nyumbani

Ukacheke na mumeo mama umpumbaze chumbani...

Wakaja shemeji zako uwaweke barazani

Chanzo: Mwamzandi (2002)

Katika mishororo hii, inathibitika kwamba makaribisho nyumbani yanategemea zubu alilonalo mtu au kukosekana kwake. Wanasaikolojia wametuambia kuwa mwanamke hashabihiani na mwanamume kwa kuwa amehasiwa tangu kuzaliwa kwake. Hana zubu na hii ndiyo sababu inayotajwa ya mtoto wa kike kutamani kuwa na zubu kuliko uchi alionao. Tunapotafakari hilo, tunaona kwamba mwimbaji anajaribu kumuasa bibi harusi juu ya umuhimu wa kupima jinsi zubu linavyoweza kumwathiri iwapo hatafuata wasia unaotolewa.

Mwanzo kabisa, bibi harusi anahimizwa amkaribishe mumewe chumbani. Chumba hiki kimetumika kama taswira ya uchi wa mwanamke. Kama ilivyo tupu ya mwanamke ya kupokea zubu la mwanamume, chumba kinaweza kutafsiriwa na wanasaikolojia kama mfano wa tupu ya kike (taz. Tyson, 2006: 20). Hii ndiyo sababu labda pakawa mahala maalumu pa mwanamke pa kumpokea mumewe. Humo, mwanamke anahimizwa “acheke” na “kumpumbaza” bwana harusi ambaye atakuwa mumewe baada ya muda mfupi. Rai inayotolewa na wimbo kwa bibi harusi kupitia maneno “ukacheke” na “umpumbaze” haikutumika **kisadfa** ila inanasisitiza kuwa pindi tu bibi harusi anapokwenda nyumbani kwake, basi atumie chumba chake kwa ajili ya kumstarehesha mume. Chumba chake na zubu la mume ni haki yake na asichelee kuhakikisha kuwa mume amepata haki yake ya ndoa.

Comment [WU1]:

Ni dhahiri katika wimbo huu kuwa mbali na mume, wapo wanaume wenye mazubu yanayostahili kuepukwa. Hawa ni wanaume ambao wako daraja moja na bwana harusi na wana uwezo wa kuanzisha uhusiano usiokuwa stahiki. Katika mahusiano ya wanawake na wanaume, wahusika wanaostahili kuepukwa kwa kuwa ni wanaume wenye mazubu “hatari” kwa bibi harusi (isipokuwa bwana harusi mwenyewe) ni shemeji zake bibi harusi. Bibi harusi anashauriwa awaweke jamaa hawa barazani. Tunavyofahamu, baraza za nyumba za Waswahili huwa nje. Hawa wana mazubu yasiyoweza kudhibitiwa na wako daraja sawa na kaka yao. Ushauri wa kuwaweka nje unafafanua namna wanavyostahili kuhusiana na mke wa kaka yao. Kufanya kinyume na maagizo haya huenda kukawa sababu ya kudhaniwa kwa bibi harusi kuwa ni mwasherati au anayeendeleza uhusiano wa ngono na shemeji zake. Wimbo unasisitiza hili ili kumkomaza mwari mapema kabla haijamsibu hatari.

2.2 Mawifi na Mashoga: Wanawake Wenye Mazubu?

Wakaja mawifi zako mama uinuke kitandani...

Wakaja mashoga zako sema nao dirishani

Chanzo: Mwamzandi (2002)

Mawifi, au dada zake mume, wana hadhi ya kipekee wanayotengewa katika wimbo. Tumeona hapo juu kwamba kaka zake bwana harusi au shemeji zake mke wamewekwa upenuni kwa sababu ya kuwa na mazubu. Mawifi hata hivyo ndio watu wa pekee waliopewa nafasi ya kukaribishwa na kuingia chumbani mwa kaka yao. Wanaruhusiwa kuingia chumbani kwa kuwa ni “wanaume” kama alivyo kaka yao ila wakati huu hawawezi kumdhuru wifi yao kwa kuwa hawana mazubu. Hawa hawawezi kuwa tishio kwa wifi yao kutokana na nasaba ya kidamu inayomzuia kaka yao asiwe na uhusiano wa aina yoyote wa kingono nao. Bwana harusi, katika muktadha huu, naye analo zubu ingawa amehasiwa kutokana na mahusiano ya kidamu na dada zake.

Katika kundi hili la wanawake wenye mazubu, kuna mashoga (marafiki) ambao bibi harusi anashauriwa asiwaingize nyumbani (kwa hofu ya kumpokonya mume). Hawa wamepea katika fani ya mapenzi na ndiyo sababu inayowafanya mwimbaji, somo na kungwi wamhimize bibi arusi aseme nao “dirishani.” Dirisha limetumika kisitiari kurejelea haja ya kuwa mbali nao. Kama walivyo shemeji kwa bibi harusi, mashoga wana uwezo sawa wa kuivuruga ndoa iwapo hawatawekwa mbali na alipo bwana harusi. Hawa aghalabu wanafahamu siri nyingi za bibi harusi na huenda wakawa chanzo cha kumchukua mume na kumfanya kuwa wao.

Tunaweza kutafsiri kuwa mashoga wana mazubu yanayowapa uwezo wa kumwoa bibi harusi. Huenda mashoga wakamchukua bibi harusi kuwa mke wao kwa kuwa wameshakuwa wanaume japo hawana mazubu. Ile hali ya

mashoga kuweza kuolewa na yule mume ni ishara ya kumuoa yule mke. Hii ni kwa sababu katika macho ya mashoga yule mume ni mke kwao na bwana harusi huweza kuwa windo kwao. Kama alivyo bibi harusi ambaye kwa wanaume Waswahili hutongozwa hadi akamkubali bwana harusi kuwa mumewe, bwana harusi naye vilevile anaweza “kutongozwa” na mashoga akawa “mke” nyumbani. Hii ndiyo sababu ya kutolewa kwa tahadhari hii, hasa kwa wanawake walioolewa mijini:

*Nasema na kina dada mnaokaa mjini
Nye mnao waume leo sikizeni kwa makini
Karandinga limelia vibaibui begani
Muwazuwie waume wasirande majiani
Muwafunge kwa vitanzi muwafiche maziwani
Akija akikutoka mume humuoni asilani
Atapikiwa mkate na vichuzi bakulini
Atafukizwa na udi na asumini kitandani
Atakupita na Honda “Yule si Bwana Khalfani?”
Utolewe gwanda lako ulie na mito kitandani*

Chanzo: Mwamzandi (2002)

Ile dhana ya kuwaficha wanaume “maziwani” ni ishara ya kuwalinda wanaume wasije “wakaolewa” na mashoga ambao kazi yao kubwa ni “kuwawinda” wanaume na kuwageuza kuwa wao. Mashoga ni wakakamavu na wanazijua mbinu mbalimbali za kuwachangamkia wanaume. Bwana harusi, pamoja na kumiliki zuby hana pingamizi kwa mashoga zake bibi harusi. Kama atavyowekwa bibi harusi kinyumba na mumewe mtarajiwa, ndivyo bwana harusi naye atakavyowekwa nyumbani na kuengwaengwa na mashoga. Hapa tunaieleza namna bwana harusi atakavyodanganywa na “vichuzi bakulini” na “kufukizwa udi na asumini” ili aiache ndoa yake ya awali kwa kufukuzia ndoa hii mpya inayomuahidi mambo mazuri. Hatima ya hayo ni bibi harusi “kupitwa na Honda” na kubakia akiuliza “Yule si Bwana Khalfani?” Swali hili la kibalagha linakariri namna bwana harusi anavyoweza “kuolewa” na mashoga zake bibi harusi kiasi cha kutojali ndoa yake ya awali. Na hii ni tahadhari kwa bibi harusi ya umuhimu wa kuachana na mashoga pindi tu anapoolewa.

2.3 Ndugu Waliohasiwa/Wenye Mazubu Butu

*Wakaja na ndugu zako uwakaribishe nyumbani...
Wanapokuja wakwezo uwaweke ukumbini*

Chanzo: Mwamzandi (2002)

Wapo wanaume ambao ijapokuwa wana mazubu, kamwe hawawezi kuwa na uhusiano wa kingono na bibi harusi ama kwa sababu ya kuhasiwa na kuzaliwa wanawake au kwa sababu ya uhusiano wa kidamu. Ndugu zake mke, wa kike na wa kiume, wanapata hifadhi ndani ya nyumba kwa kuwa si tishio kwa bibi harusi kwa mumewe. Wahusika hawa wana hadhi sawa na wakwe (wazazi wake mume). Hawa, inavyobainika, hawawezi kumtaka kimapenzi bwana na bibi harusi.

3.0 Ung'amuzi Jumuishi na Jinamizi la Woga katika Nyimbo Teule

Carl Gustav Jung (1895-1961) ni mwanafunzi wa Sigmund Freud na anahusishwa sana na fikra aliyoiendeleza ya “ung'amuzi jumuishi” inayodai kuwa binadamu wote, popote walipo duniani hufanana (Wamitila 2003: 298). Katika nadhariatete zake Jung, kwa mfano, anaamini kuwa binadamu wote hutawaliwa na woga ambao huwa umefichika ndani ya ung'amuzibwete wao. Mtaalamu huyu anazungumzia kuwapo kwa ngano za majitu na viumbe wa kutisha katika jamii nyingi duniani kama mfano wa ung'amuzi jumuishi wenye ubia na unaowafanua binadamu (Schmitz, 2007). Maoni haya ya Jung yanaweza kuwa na chembechembe za ukweli hasa tunapozingatia jinsi nyimbo teule za harusi zinavyowatia hisia za woga bwana na bibi harusi. Pengine kwa kufahamu kuwa binadamu wamefutika sifa za woga kwenye ung'amuzibwete wao, nyimbo hizi hujaribu kuwafanya bwana na bibi harusi waione ndoa na matarajio yake kama kitu kinachostahili kuogopwa. Hata hivyo, matarajio ya Waswahili katika nyimbo hizi si woga halisi; badala yake, maharusi wanatarajiwa wawajibikie ipasavyo mahitaji na matarajio ya kimwili katika ndoa yao. Kwa yakini, matusi yaliyomo yanaweka wazi umuhimu huu wa kutoona haya wala vibaya katika kuiwajibikia ngono.

4.0 Viashiria vya Zuby na Athari zake katika Nyimbo za Harusi

Baadhi ya wafeministi wamelitaja zuby kama sehemu ya siri na ya kiyakinifu inayochukuliwa kama kifaa cha kumdhuru mwanamke (Tyson, 2006). Viashiria vyake vinakaribiana sana na kile ambacho wanasaikolojia changanuzi wangependekeza tutafute pindi tunapofasiri taswira za zuby katika ndoto. Wanasaikolojia hutuhimiza tutafute taswira za minara, mishale, ndege aina ya “*rocket*” na hata majambia (Tyson, 2006: 20). Kwa kuwa umbile la kibiojia la mwanamke huwa linapokea tupu ya mwanamume, nyimbo husika husawiri mapokezi hayo kama adhabu kali anayopewa mwanamke.

4.1 Viashiria vya Zuby na Umbo la Mche

Sawa na anavyohimiza Tyson (2006), nyimbo kadhaa zilizochanganuliwa katika sehemu hii zina maumbo mbalimbali ya zuby ambayo yanafanana na minara, mishale na ndege aina ya *rocket*. Maumbo hayo ya zuby yamechukua

maumbo ya mche kama vile mtaimbo, fimbo na hata kisiki katika nyimbo mbalimbali za Waswahili. Tazama mifano ya nyimbo hizi:

Mtaimbo

Hauna eeh

Hauna laika

Eeh laika eeh

Ooo hauna huo

Hauna laika

Naupeleleza mtaimbo

Unateleza mtaimbo

Mtaimbo wa zamani

Unateleza mtaimbo

Mtaimbo oooh mtaimbo

Hautaki kulala

Hauna laika

Ni kipara huo

Hauna laika

Mtaimbo oooh mtaimbo

Nalia yomi kikumbuka mtaimbo wangu nalia

Nalia yomi kikumbuka mtaimbo wangu nalia

Mtaimbo wa ajabu

Unateleza mtaimbo

Chanzo: Ali (2014)

Wimbo huu unazungumzia “mtaimbo” au chuma kirefu kinachotumiwa kufanyia kazi za shokoa kama vile kufua nazi au hata kuchimbia mawe timboni. Kwa hakika, wimbo unafafanua sifa za uchi wa mwanamume, yaani zuby na matarajio yake katika jamii. Vipo vidokezo mbalimbali vinavyobainisha kuwa huu ni uchi wa mwanamume vikiwamo namna mtaimbo “unavyoteleza” (unapoingia tupu ya mwanamke), usivyokuwa na laika (yaani usivyokuwa na nywele, na hivyo basi kuteleza kwa urahisi), usivyotaka kulala (uchi adili ni ule uliosimika daima dawamu, tayari kufanya kazi yake), ulivyo na kipara (sehemu ya zuby ambayo ni sawa na kichwa kilichonyolewa), miongoni mwa sifa nyinginezo. Hebu tazama sasa namna bibi harusi (pengine na watu wake) anavyotishwa na “mtaimbo” katika wimbo huu wa “Keshauona.”

Keshauona

Alipouona Harusi wenu alikwenda mbio

Ah! Ah! Eee si ajabu tena

Mtaimbo keshauona

Chanzo: Ali (2014)

Katika wimbo huu, bibi harusi (na watu wa aila yake) wanafanyiwa stihizai za wazi kuwa ni waoga. Wimbo huu, ambao huimbwa pindi harusi inapojibu au pale bibi harusi anapobainika kuwa ni bikira, unatoa wazo kuwa bibi harusi alipata tabu kuvumilia kitendo cha ngono na bwana harusi. Anasawiriwa kama mwoga mkubwa aliyetoroka pindi tu alipoliona zubu la bwana harusi ambalo lilidhamiria kumuumiza.

4.2 Zubu kama Fimbo ya Kutoa Adhabu

Fimbo, halikadhalika, ina umbo la mche. Huwa nyembamba na hutumika kama kifaa cha kuwachapia watu. Fimbo inayozungumziwa inahusu namna tendo la ngono linavyogeuka kuwa adhabu kwa mwanamke. Mwanamke, yaani bibi harusi, akiwa “mpokeaji” wa adhabu analalamika kutokana na adhabu za zubu lisilokimwa wala kutosheka. Wimbo huu wa “Fimbo” unazungumzia kwa siri jinsi mwanamume (bwana harusi) anavyoweza kuwa na ashiki zisizoisha au la mwanamke (bibi harusi) amzuie asiendelee kumuumiza.

Fimbo

Wacha kukoroma aah bwana wacha kukoroma

Fimbo ya kwanza aah hewalla bwana

Fimbo ya pili aah hewalla bwana

Fimbo ya tatu aah hewalla bwana

Fimbo ya nne aah hewalla bwana

Fimbo ya tano aah hewalla bwana

Fimbo ya sita aah hewalla bwana

Fimbo ya saba aah hewalla bwana

Fimbo ya nane aah hewalla bwana

Fimbo ya tisa kumanina unaniumiza mtwana.

Chanzo: Ali (2014)

Katika wimbo huu, hesabu za fimbo (kuanzia ya kwanza hadi ya tisa) ni matokeo ya uchu wa mwanamume uliokithiri na hiyo ni sababu tosha ya kumtia woga mwanamke (Ali, 2014). Mwanamume huyu amemwingilia mkewe anayemridhia hadi inapofika mara ya tisa ambapo anamtusi mumewe na kumwambia anamuumiza. Bibi harusi anaambiwa, walau kwa mafumbo, kuwa wapo wanaume kama hawa ambao ashiki zao zina uwezo wa kusababisha karaha.

4.3 Zubu kama Kitu cha Kuchoma

Katika wimbo wa “Kimenichoma” twapata tena taswira ya zubu iliyofichwa na kisiki cha mpera. Kwa Waswahili, mpera ni miongoni mwa miti migumu na binafsi nakumbuka tulitumia visiki vya mpera kama zana ya kufulia nazi. Ugumu huu ndio unaorejelewa na bibi harusi; anatishwa kwamba atapata hatima ngumu ya “kufuliwa” na zubu. Wimbo unatueleza:

Kimenichoma

Kimenichoma eee kimenichoma

Kisiki cha mpera

Wapi?

Hapa

Patie dawa sana pasije pakabana

Pakamkera bwana

Usiku na mchana

Chanzo: Ali (2014)

Tunadokezewa namna zubu linavyoweza kuchoma na kusababisha athari ya ndwele ambayo kupona kwake kutahitaji kidonda kilichosibu kupakwa dawa.

4.4 Mwanamume Mwoga

Nyimbo za kumsimanga mwanamume si nyingi na zilizopo hujaribu kumshajiisha kutimiza kitendo cha ndoa. Atakayeshindwa kutekeleza hilo anauhatarisha uume wake. Kuwa mwanamume wa kweli basi ni kujishajiisha kwa bwana harusi asiwe sawa na mwanamume aliyehasiwa. Wimbo “Mume Mwoga” unaweka wazi stihizai anazofanyiwa bwana harusi:

Mume Mwoga

Mume muoga mkimbia ng’ombe

Sitamwoza mwanangu.

Chanzo: Ali (2014)

Wimbo huu aghalabu huimbwa pale bwana harusi anapoingia chumbani mwa bibi harusi huku watu wakiwa na mshawasha wa kujua iwapo bwana harusi ataweza kutimiza tendo la ngono kwa mara ya kwanza na mkewe halali. Hutokea wakati mwingine mabwana harusi wasiweze kutekeleza hilo kwa kuhisi woga. Bwana harusi kama huyu ndiye anayesimangwa kama “mkimbia ng’ombe” yaani mtu anayehesabiwa kuwa mwoga asiye na thamani. Ng’ombe, tunavyofahamu, hawezi kumdhuru mtu na hivyo basi haijuzu kwa mwanamume wa kweli kutishwa na ng’ombe. Bwana harusi anayeshindwa kumwingilia bibi harusi katika muktadha huu huonekana kama asiye na thamani na anatishwa

kuwa kushindwa kutekeleza tendo la ngono kutamfanya asiozwe mke huyu aliyemchagua mwenyewe. Kwa hivyo, mwanamume wa kweli sharti ajikaze asije akashindwa kutekeleza wajibu huu.

Wakati mwingine kule kumiliki zubu kwa mwanamume hakutoshi kwa kuwa wanawake nao hujali sana kuwapo kwa sifa maalumu za zubu hilo. Wanawake huolewa wakitarajia waume waliohitimu katika fani ya mapenzi kwa kuwapa haki zao za ndoa. Wimbo huu wa “Acha Kukoroma” unawasilisha sifa za wanaume butu:

Acha Kukoroma

*Kila nikikuita wanyamaza kimya eee
Chukua mapumbu uyaweke nyuma
Wacha kukoroma bwana vitombe kuma
Na mkuma wangu nimeusugua
Na mavuzi yangu nimeyanyonyoa
Wacha kukoroma vitombe kuma*

*Ashin ashin nalidhani mboo kumbe msuwaki
Ati we mkuma wangu nimeusugua vyema
Wacha kukoroma vitombe kuma
Mume wangu wangu simwambii nacha
Kila vijiti na utamu wake*

Chanzo: Ali (2014)

Kama mada ya wimbo inavyodokeza, mwanamume anayesimangwa hapa hustahabu kulala kuliko kuyakidhi mahitaji ya kimwili ya mkewe. Mume huyu analala kiasi cha kukoroma huku akisahau wajibu wake. Anasutwa aache kukoroma na atende kile mwanamke anachokitaka hapo kitandani. Taswira inayojitokeza hapa ni kuwa huyu ni mwanamume aliyehasiwa na zubu lake mwenyewe. Kilicho mbele si zubu ila ni “mapumbu” ambayo anashauriwa ayaweke nyuma. Hata mapumbu yanapowekwa nyuma, kilichobakia hakiwezi “kuadhibu” kama linavyotarajiwa zubu. Badala yake, kilichopo ni “mswaki” ambao hauwezi kuadhibu uchi wa mwanamke kwa kishindo kinachotarajiwa. Kwa bwana harusi, hizi ni kauli ambazo zinamsimanga na kumtia hofu iwapo atakuwa na zubu la kuadhibu au la kuchekelewa na wanawake, akiwamo mkewe.

5.0 Hitimisho

Makala haya yamechanganua uamilifu wa zuby kama kiungo halisi kinachofafanua mahusiano kati ya wanawake na wanaume katika jamii ya Waswahili. Mahusiano hayo yamebainisha kuwa wale wenye mazuby (wanaume) wanapewa mamlaka zaidi kuliko wale wasiokuwa nayo (wanawake). Aidha, imebainika pia kuna baadhi ya wanajamii ambao, ingawa hawana mazuby, wanaelekea kuwa na nguvu zaidi kutokana na mahusiano yao ya kidamu na wenye mazuby. Vilevile, wapo wenye mazuby ambao huelekea wamehasiwa na mahusiano hayohayo ya kidamu. Makaribisho ya wageni anayofunzwa bi arusi ni sitiari tu ya namna mahusiano haya ya kimamlaka kati ya mwenye zuby na asiyekuwa nalo yanavyodhihirika katika jamii ya Waswahili. Aidha, zuby limebainika kama kiungo cha kukuza na kuendeleza woga na hofu miongoni mwa wanajamii. Azma kuu hata hivyo ni kuwakomaza maharusi ili waweze kuyakabili majukumu yao mapya – ya kuwa mke na mume katika ndoa.

Marejeleo

- Ali, A.H.T. (2014). "Taashira na Utendaji katika Nyimbo za Harusi za Waswahili Kisiwani Zanzibar," *Tasnifu za Uzamivu* (Haijachapishwa), Chuo Kikuu cha Egerton, Kenya.
- Burman, E. & M. MacLure (2005). "Deconstruction as a Method of Research," katika Bridget Somekh & Cathy Lewin (wah.) *Research Methods in the Social Sciences*, New Delhi: Vistaar Publications, kur. 284-292.
- Carter, D. (2006). *Literary Theory*. Reading: Cox & Wyman.
- Grosz, E. (1990). *Jacques Lacan: A Feminist Introduction*. London: Routledge.
- Lytard, J-F. (1984). *The Postmodern Condition. A Report on Knowledge*. Tafsiri ya Geoff Bennington & Brian Massumi. Minneapolis: University of Minnesota Press.
- Mwamzandi, I.Y. (2002). "Majadiliano katika Umalenga wa Kiswahili: Mfano wa Taarab," *Tasnifu ya Uzamivu* (Haijachapishwa), Chuo Kikuu cha Egerton, Kenya.
- Ntarangwi, G.M. (1998). "Taarab Texts, Gender and Islam in an Urban East African Context: Social Transformation among the Swahili of Mombasa, Kenya," Unpublished Ph.D. Dissertation, University of Illinois.
- Schmitz, T.A. (2007). *Modern Literary Theory and Ancient Texts: an Introduction*. Malden: Blackwell Publishing.
- Selden, R., P. Widdowson. & P. Brooker (2005) *A Reader's Guide to Contemporary Literary Theory (5th Edition)*. Great Britain: Pearson Education Limited.

- Tyson, L. (2006). *Critical Theory Today*. New York: Routledge & Taylor and Francis.
- Wamitila, K.W. (2003). *Kamusi ya Fasihi: Istilahi na Nadharia*. Nairobi: Focus Books.